

NEW

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na. DCC/CF.10/3

06/09/2024

TANGAZO LA AJIRA YA MUDA

Mkurugezi wa Jiji la Dar es Salaam anawatangazia
Watanzania wote wenye sifa kuomba kazi kwa nafasi
zifuatazo:-

ASKARI MGAMBO (NAFASI - 317)

MASHARTI KWA UJUMLA:

- Awe raia wa Tanzania
- Awe amehitimu Kidato cha nne au sita
- Awe na kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa
- Awe na uwezo wa kuongea lugha ya Kiswahili na Kiingereza
- Awe na afya njema kimwili na kiakili iliyothibishwa na Daktari wa Serikali
- Awe hajawahi kutumia dawa za kulevya
- Awe tayari kufanya kazi za Mgambo mahali popote ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

1

NEW

NEW

- Asiwe na kumbukumbu za uhalifu
- Awe na mafunzo ya JKT au Mgambo
- Awe na barua ya mdhamini mwajiriwa wa Serikali na mdhamini mwananchi mwenye makazi ya kudumu ya eneo husika
- Mwombaji hatakiwi kuwa na kosa lolote la madai au jinai
- Awe na umri kati ya miaka 18 – 45
- atakayewasilisha taarifa na sifa za kughushi mwombaji atachukuliwa hatua za kisheria
- Watumishi waliopunguzwa kazi/ kufukuzwa kazi /Kuachishwa kazi kwa sababu ya kughushi vyeti serikalini hawaruhusiwi kuomba.

KAZI/MAJUKUMU.

Kulinda mali za Soko, Operesheni na Malindo katika Ofisi za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

Kuhakikisha eneo analolinda linakuwa na hali ya utulivu wakati wote

Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Msimamizi wake

NEW

NEW

6. Ajira ni ya mkataba wa miezi mitatu [3].
7. Mwijiri atalipa mshahara wa Tshs. 10,000/= [Shilingi elfu kumi tu] kwa siku yenye kuleta jumla ya 300,000/= [Shilingi laki tatu tu] kwa mwezi.

Barua zote ziambatane na nyaraka zifuatazo:

Nakala za vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa ambayo ni:

- Cheti cha kidato cha nne
- Cheti cha Taaluma
- Cheti cha Kuzaliwa.
- Kitambulisho cha Taifa
- Picha ndogo za rangi (colored Passport size mbili

(2) za mwombaji za hivi karibuni).

Waombaji wenye sifa pungufu au zaidi na zilizotajwa hapo juu hawaruhusiwi kuomba kwani maombi yao hayatafanyiwa kazi.

Barua ambazo hazikuambatanishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu hazitashughulikiwa.


JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu zitumwe kwa anuani ifuatayo hapa chini na zitapokelewa Karakana ya Halmashauri ya Jiji (DEPO).

Mkurugenzi wa Jiji
1 Mtaa wa Mission
S.L.P. 20950
Halmashauri ya Jiji
11883 – DAR ES SALAAM

NEW

NB: Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 18 Septemba, 2024.saa 9.30 alasiri.


Elihuruma Mabeya
MKURUGENZI WA JIJI

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI DAR ES SALAAM

OFISI YA MKURUGENZI, 1 MATAA WA MISSION, S.L.P 20950, 11883 DAR ES SALAAM, SIMU NA 2128800, 2128805, Tovuti:
www.dcc.go.tz, Barua Pepe: info@ilalamc.go.tz